


# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA



Barabara ya Moshi Nairobi  
S. L.P 1055  
23103 ARUSHA  
Barua pepe: [rbcarusha@pcb.go.tz](mailto:rbcarusha@pcb.go.tz)  
Wavuti : [www.pccb.go.tz](http://www.pccb.go.tz)

---

ARUSHA – APRILI 11, 2019

### TAARIFA KWA UMMA

#### TAKUKURU YAFICHUA MADUDU YA OBC (OTTERLO BUSINESS CORPORATION LIMITED)

TAKUKURU (M) Arusha katika kipindi cha Mwezi Januari – Machi 2019, imefanya uchunguzi na kubaini kampuni ya Otterlo Business Corporation Limited (OBC) kupitia kwa Mkurugenzi wake Bw. Isaya Lesion Mollel imekuwa ikijihusiha na vitendo vya Rushwa ikiwemo kukwepa kodi na kuwahonga maafisa mbalimbali wa serikali kwa lengo la kuwafanya wawe watetezi wake katika mgogoro wa matumizi mseto katika Pori Tengefu la Loliondo. TAKUKURU imebaini hasara iliyosababishiwa serikali na kampuni hiyo kwa njia mbalimbali ikiwemo kukwepa kodi ni zaidi ya **Tsh 8.2 Billioni** Hivyo Mkurugenzi wa Kampuni hiyo Bw. Isaya Lesion Mollel na washirika wake walioshirikiana kutenda makosa hayo wamefikishwa mahakamani na wengie wataendelea kufikkishwa.

#### **Ndugu Wanahabari;**

Kwa kipindi tajwa TAKUKURU (M) Arusha imeendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi kama ilivyoainishwa kwenye Sheria ya kuzuia na kupambana na Rushwa Na. 11/2007 kama ifuatavyo;

#### **1. UCHUNGUZI NA MASHITAKA :**

##### **A. TAARIFA ZILIZOPOKELEWA**

Kwa kipindi tajwa zilipokelewa taarifa **138** kutoka sekta mbalimbali kama ilivyo katika jedwali lifuatalo;

Na	SEKTA	IDADI
1	Halmashauri	66
2	Elimu	18
3	Mahakama	13
4	Polisi	12
5	Ardhi	4
6	Afya	4
7	Kilimo	3
8	Idara ya Kazi	3
9	Magereza	2

10	Madini	2
11	Maji	2
12	TANAPA	2
13	NCAA	2
14	Sekta ya Utalii	1
15	TANESCO	1
16	TEMDO	1
17	TRA	1
18	Misitu	1
<b>JUMLA</b>		<b>138</b>

Taarifa hizi zilipelekea kufunguliwa kwa majalada 32 ya Uchunguzi na yanaendelea kuchunguzwa na chunguzi zake zipo katika hatua mbalimbali. Pia ushauri yakinifu umekuwa ukitolewa kwa watoa taarifa kwa malalamiko yanayoonekana kutoangukia kwenye sheria yetu.

#### B. KESI MAHAKAMNI

Kwa kipindi tajwa, TAKUKURU (M) Arusha imefungua mashitaka mapya kumi na moja (11) mahakamani.

Aidha hadi sasa jumla ya mashauri thelathini na tisa (39) yanaendelea mahakamani yakiwa katika hatua mbalimbali za kimahakama. Pia kwa kipindi hicho tumeshinda Mashauri matatu (3).

#### 2. UFUATILIAJI WA FEDHA ZA UMMA KWENYE MIRADI YA MAENDELEO

TAKUKURU (M) Arusha kwa kipindi tajwa imefanya ufatiliaji wa matumizi ya fedha za umma katika miradi miwili (2) ambayo serikali imewekeza fedha jiasi cha **Tsh 844,955,902.7/=**.

Miradi iliyofuatiliwa ili kuthibitisha thamani ya fedha iliyotumika (Value for Money) ni;

- a. Mradi wa Maji katika Kijiji cha Malambo(Ujenzi wa Tenki la maji,Manywesheo ya mifugo na utandazaji wa mabomba) wenye thamani ya **Tsh 634,769,402.70/=**, mradi huo bado upo katika hatua za utekelezaji na hadi sasa kiasi cha **Tsh 343,734,908.68** kimeshalipwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo.
- b. Ukarabati wa miundombinu ya barabara za Wasso – Sakala – Loliondo, Loliondo Olmesuit na Olorien/Magaiduru – Mageri wenye tamani ya **Tsh 210,186,500/=**, mradi huo bado upo katik utekelezaji na hadi sasa kiasi cha **Tsh 53,467,500/=** kimeshalipwa kwa ajili ya utekelezaji.

### 3. ELIMU KWA UMMA:

TAKUKURU (M) Arusha imeendelea kufanya jitihada za kuelimisha Umma uelewa mpana wa dhana ya Rushwa na pia kuwakumbusha wajibu wao katika mapambano dhidi ya Rushwa. Kama inavyofahamika kuwa mwaka huu ni mwaka wa uchaguzi hivyo elimu yetu imejikita sana katika kuelimisha umma na juu ya wajibu wao wa kuchagua viongozi wanaofaa na sio watoa Rushwa. Katika kipindi tajwa yafuatayo yamefanyika;

Na	KAZI ILIYOFANYIKA	IDADI
1	SEMINA	101
2	MIKUTANO/MIJADALA	130
3	KUFUNGUA KLABU	54
4	KUIMARISHA KLABU	210
5	MAONYESHO	9
6	UANDISHI WA MAKALA	18
7	VIPINDI VYA REDIO	12
8	TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI	5
9	UGAWAJI WA VIPEPERUSHI MBALIMBALI	2,280

TAKUKURU Mkoa wa Arusha inawashukuru wananchi wa Mkoa wa Arusha kwa Ushirikano wanaoutoa kwa Taasisi yetu kwa kutoa taarifa za wanaojihusha na vitendo vya Rushwa na kuwataka kuendelea na moyo huo. TAKUKURU inawahakikishia kuwa taarifa zitakazopokelewa zitafanyiwa kazi kwa haraka.

Mwisho TAKUKURU Mkoa wa Arusha inawaonya watu wote na watumishi wa Umma wanaotumia nafasi zao kujipatia manufaa wasiostahili na hivyo kuisababishia serikali hasara kuacha kufanya hivyo mara moja vinginevyo watakutana na mkono wa sheria.

Aidha tunawaasa wananchi kutokubali kununuliwa katika kipindi hiki cha uchaguzi kwa kuwa viongozi wanaopatikana kwa njia za Rushwa hawafai na hawaitakii mema nchi yetu.

*Penda nchi yako, kataa rushwa*

*Asanteni kwa kunisikiliza*

**Imetolewa na:**

**FRIDA WIKESI,  
KAIMU MKUU WA TAKUKURU (M) ARUSHA**